

WASISRA ATIBUA MITANDAO 2015

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Stephen Wassira, anadaiwa kutibua mitandao ya makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliojipanga kuusaka Urais wa mwaka 2015 kupitia chama hicho, *Tazama Tanzania* limeelezwa.

Habari za uhakika zilizopatikana kutoka mikoa inayounda Kanda ya Ziwa, zimetaja mwanasiasa huyo mkongwe nchini kwamba kwa sehemu kubwa amekuwa kikwazo kwa baadhi ya mitandao kujijenga katika ukanda huo.

Kanda ya Ziwa inatajwa kuwa moja ya kanda muhimu katika mbio za urais, ambayo imekuwa ikifanikisha ushindi wa si tu kwa wagombea urais, bali wote wanaosaka nafasi za juu za uongozi ndani ya CCM, na hasa ujumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) Taifa.

Kwa mujibu wa Habari hizo, Wassira ametajwa kuwa kikwazo kikuu kwa baadhi ya Makada wa CCM wenye nia ya kugombea urais mwaka 2015, baada ya wasimamizi wa mitandao hiyo kutakiwa kuweka msimamo wao wazi kwanza kama nao wako tayari kumuunga mkono mwanasiasa huyo endapo na yeye ataamua kujitosa katika kinyang'anyiro hicho cha urais.

Wassira anatajwa kukubalika kwa kiasi kikubwa katika ukanda huo wa Kanda ya Ziwa, na kwahiyo wengi wa wanamitandao ya urais 2015 wamekuwa wakipigana vikumbo kumtaka awaunge mkono katika mbio zao hizo, ili kupitia kwake waweze pia kuungwa mkono na wajumbe wa vikao vya uteuzi kutoka kanda hiyo.

Hata hivyo, gazeti hili limeambiwa kwamba matokeo ya vikumbo hivyo vya wanamitandao hiyo ya urais katika kanda hiyo ya Ziwa, yamekuwa si ya kuridhisha baada ya kubainika kuwa hata Wassira mwenyewe anayo nia ya kugombea urais mwaka 2015 ingawa yeye binafsi hajaweka wazi nia yake hiyo.

Kutokana na hali hiyo, imeelezwa kwamba makada wote wa CCM wanaokwenda kutafuta uungwaji mkono katika kanda hiyo, wamekuwa wakipewa sharti linalowataka na wao wakubali kufanya kazi ya ziada kuwashawishi wajumbe kutoka katika kanda zao wamuunge mkono Wassira endapo naye ataamua kuweka jina.

“Unajua, harakati za kusaka urais ndani ya CCM lazima zijikite katika pande zote za nchi hii, lazima uwe na watu maalumu kutoka kila kanda maarufu. Ukiacha kanda ya Ziwa, zipo pia kanda ya kusini, kanda ya nyanda ya juu kusini, kanda ya kati, kanda ya Pwani na kanda ya kaskazini” anasema mtoa habari wetu mmoja kutoka kanda ya ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera.

Anaongeza : “Lakini katika kanda zote hizo, Kanda ya Ziwa mara nyingi ndiyo imekuwa ikitajwa kama kanda ya ushindi, Tangu enzi za kusaka Uhuru, enzi za Mwinyi, Mkapu na hata Rais Kikwete mwenyewe, wote walihakikisha kwamba wanakubalika kwanza kwa wajumbe wa kanda hii.

“Hata Marais wa Zanzibar, ili ujhakikishie uteuzi ndani ya vikao vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu, lazima karata zako uzicheze kwa kuhakikisha unao watu wa kukusemea kutoka kanda ya Ziwa. Ukishakuwa na wajumbe wawili, watatu wanaoheshimika katika ukanda huu, na ambao wanaweza kusimama na kukusemea ndani ya vikao vya Uteuzi, unakuwa umemaliza kazi.

“Kwasasa, Wassira anakubalika na kuheshimiwa sana na wajumbe wa NEC na hata wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Mara Kagera na Shinyanga. Ukiwa na mtandao wako wa urais na ukafanikiwa kumweka mikononi mwako Wassira, umemaliza kazi.

“Ndiyo maana safari za wanaosaka urais wa 2015 haziishi hapa Mwanza mikoa mingine ya kanda hii, ingawa mambo hayawaendei kama walivyotarajia kwasababu ya Wassira. Huenda Wassira akachukua fomu ya kugombea Urais 2015, kwahiyo kila mwenye mtandao wake anayetaka ‘sapoti’ yake, lazima na yeye akubali kumsapoti endapo atachukua fomu, vingivyo wenye mitandao yao watakwaa kisiki”

Wassira na Mwenyekiti wa sasa wa CCM Mkoa wa Mwanza, ANTONY Diallo, wanatajwa kuwa mhimili mkuu wakati wa mtandao wa Rais Jakaya Kikwete katika kanda ya Ziwa.

Mtandao uliomwingiza Rais Kikwete Ikulu, ukiacha kanda hiyo ya Ziwa ulijiimarisha pia katika kanda za kaskazini, nyanda za juu kusini, kanda ya magharibi, kanda ya kati, kanda ya kusini na kanda ya Pwani.

Edward Lowassa, pamoja na kuratibu Mtandao wa Rais Kikwete kitaifa, alihakikisha pia anawaunganisha wajumbe wa vikao vya uteuzi kutoka kanda ya kaskazini ili wamuunge mkono mtu wao huyo, kama ambavyo Benard Membe, Juma Jamaldin Akukweti (sasa ni marehemu) na Dk. Emmanuel Nchimbi walivyohakikisha wanaunganisha nguvu zao katika mikoa inayounda ukanda wa kusini.

Yusuf Makamba, ambaye baadaye alikuja kuwa Katibu Mkuu wa CCM mara tu baada ya Rais Kikwete kuukwaa urais na hivyo kushika pia usukani wa kuongoza chama hicho kama Mwenyekiti Taifa, na Rostam Aziz walijikita kujenga mtandao huo katika mikoa ya kanda ya kati, Pwani na Zanzibar wakati kina Samwel Sitta na Profesa Juma Kapuya waliujenga mtandao kanda ya Magharibi.

John Mwakipesile na wenzake, ambaye baadaye alikuja kuteuliwa na Rais Kikwete kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, walipewa jukumu la kujenga mtandao huo katika mikoa ya nyanda za juu kusini, wakati Charles Gishuli, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga wakati huo, alidaiwa kupewa kazi ya kuwaunganisha wenye vitu wenzake wa mikoa, Baada ya kazi yake hiyo, Gishuli alipewa ukuu wa wilaya.

Wachambuzi mbalimbali wa siasa za nchi hii, wametabiri kuwepo ugumu na mchuano mkali katika mchakato wa uteuzi wa mgombea ndani ya CCM na hata Uchaguzi Mkuu wenyewe wa

mwaka 2015 kutokana na makundi ya wanamtandao ndani ya chama tawala hicho kuukamia urais huo,na hiyo ndiyo sababu kuu inayowalazimu wenye mitandao yao kuhitaji msaada wa kuungwa mkono na mitandao mingine.

Baadhi ya wachambuzi hao wametolea mfano Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika April mwaka huu,ambapo washindani wakubwa katika nafasi ya urais ,Uhuru Kenyatta na Raila Odinga, walilazimika kuacha vyama vyao na kuunda mitandao mipya kwaajili ya kuunganisha mitandao yenye nguvu za kisiasa.

Kwa mfano ,wanasema Kenyatta ambaye alikuwa kiongozi wa KANU, baada ya kufanikiwa kumshawishi mwanasiasa mwenye mvuto katika siasa za nchi hiyo,William Ruto,walifikia muafaka kwa kila mmoja kulazimika kuachana na vyama vyaovya awali, na kuunda muungano wa Jubilee. Kabla ya hapo,Ruto alikuwa na Odinga katika chama cha ODM.

Vivyo hivyo,Odinga baada ya kufanikiwa kumvuta mwanasiasa mwingine mwenye mvuto,Kalonzo Musyoka,kwa pamoja waliamua kuachana na vyama vyao vya awali na kuunda Muungano wa CORD.

Kwa mujibu wa wachambuzi hao, hali kama hiyo ya Kenya ndiyo inayotarajiwa kujitokeza ndani ya CCM mwaka 2015, kwa wenye mitandao yenye nguvu kulazimika kuunganisha nguvu zao ili kukabiliana na mitandao mingine yenye nguvu pia.

Hadi sasa haijafahamika ni mitandao mingapi ya wanaCCM wanaousaka urais,wala mtandao wa Wassiraunaundwa na wanasiasa wakabila gani, lakini baadhi ya makada wa chama hicho,kwa kauli za wapambe wao na mwenendo wao wa kisiasa,wanaonyesha kuwa na mitandao yao tayari inayoratibiwa chini kwa chini kwa kuwatumia wana-CCM wanaounga mkono harakati zao hizo.

Hadi sasa, makada wa CCM ambao wamekuwa wakitajwa mara kwa mara katika vyombo mbalimbali vya habari kwamba tayari wanayo mitandao ya urais wa 2015, kumrithi Rais Kikwete ni pamoja na Edward Lowassa,Benard Membe,Samwel Sitta,Dk.Emmanuel Nchimbi, na Profesa Mark Mwandosya, ingawa watu walioko karibu na mwanasiasa huyo ambaye ni Waziri asiye kuwa na Wizara maalumu, wameliambia gazeti hili kwamba mtu wao huyo huenda hatachukua fomu 2015.

Kinamfanya Wassira awe kimbilio la wenye mitandao la wenye mitandao yao, na hata yeye mwenyewe kushawishika kuweka nia ya kuchukua fomu ya kuomba CCM kimteue kugombea urais, pamoja na mambo mengine, ni kukubalika kwake ndani ya chama hicho.

Katika uchaguzi mkuu wa ndani ya chama uliomalizika Novemba mwaka jana, Wassira ndiye aliyeibuka kinara kwa kuzoa kura nyingi kuliko wajumbe wengine wote waliochaguliwa na mkutano mkuu kuingia katika kikao cha NEC Taifa.

Aidha, Wassira aliongoza pia kwa kupata kura nyingi kutoka kwa wajumbe wa NEC, kuingia kikao cha Kamati Kuu, hali inayomfanya awe tegemeo kubwa kwa wanamitandao ya urais,

katika ushawishi wa wajumbe wa vikao vikuu hivyo viwili muhimu linapokuja suala la uteuzi wa mgombea urais ndani ya CCM.

Tazama Tanzania Jumanne Julai 23-29, 2013.